

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)



MAKUBALIANO YA MKATABA WA KUTENGENEZA FREMU ZA MILANGO NA "VENT" UJENZI WA CHUO CHA VETA MKINGA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 17 mwezi 1 mwaka 2022

KATI YA

Mkurugenzi wa Kanda, **VETA Kanda ya Kaskazini, S.L.P. 1738, Moshi**, ambaye anaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802, Dodoma (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja

NA

ABDUL FUNYO CO. LTD, wa S.L.P 1793, TANGA (ambaye katika Mkataba huu ataitwa "**MZABUNI**" kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri anajenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mkinga;

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Mzabuni mchanganuo wa kazi za Ujenzi vinavyoonyesha kazi zitakazofanyika.

NA KWA KUWA Mzabuni amekubali kwa hiari yake kufanya kazi ya kutengeneza na fremu za milango na "vent".

Hivyo basi pande zote mbili zinakubaliana na masharti yaliyopo hapa chini kama ifuatavyo:-

PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KWAMBA:-

1. Maelezo ya kazi:-

- 1.1. Gharama ya kutengeneza Fremu za milango na "vent" itakuwa Tzs. **35,702,800.00** (kwa maneno Thelathini na tano milioni laki laki saba na mbili elfu na mia nane na senti sifuri tu fedha za Kitanzania) kwa majengo kumi na sita (16).
- 1.2. Kwamba, Mkataba huu utakuwa wa mwezi mmoja, kuanzia tarehe utakayopokea oda (LPO).
- 1.3. Kazi itafanyika kutokana na oda (LPO) utakayopewa kwa kurejea mchanganuo wa mahitaji na bei uliyoambatanishwa.
- 1.4. Mzabuni anatakiwa azingatie vipimo kwa usahihi kulingana na maelekezo ya kazi.
- 1.5. Kama kuna mabadiliko katika Mkataba (variations), mabadiliko haya yatawasilishwa kwa njia ya maandishi na pande zote mbili zinazohusika, zitakubaliana namna ya utekelezaji wa mabadiliko hayo.

2. Kipindi cha utekelezaji:

- 2.1. Kwamba, wakati wa utekelezaji wa mkataba huu mwajiri anaweza kuongeza muda wa mkataba iwapo kutakuwa na sababu zitakazodhahirika kuwa ni sababu za msingi na zisizozuilkia.

3. Malipo kwa Mzabuni

- 3.1 Mwajiri atalazimika kumlipa Mzabuni malipo yote ya kazi aliyofanya baada ya kupata hati ya kuleta vifaa (Delivery note), hati ya madai (invoice) iliyoambatanishwa na risiti ya kielektroniki (EFD) pamoja na ripoti ya ukaguzi kutoka kamati ya mapokezi ya vifaa.

- 3.2 kwamba, Mzabuni atakiri kwa maandishi kulipwa malipo hayo ndani ya siku tatu (3) baada ya kupokea malipo.

4. Msimamizi wa Mkataba huu atakuwa Mhandisi wa mradi (Site Engineer).

5. Ubora wa kazi:

Mzabuni atatekeleza kazi kwa ubora, uaminifu na kulingana na viwango vya ubora unaokubaliwa na Mwajiri. Kazi ambayo itakuwa haina ubora na kiwango kinachohitajika na Mwajiri, itarekebishwa na Mzabuni kwa gharama zake.

6. Usalama wa wafanyakazi:

Mzabuni anatakiwa kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wake mwenyewe.

